# SALAMU MALKIA MTAKATIFU-MAMAWA HURUMA

Kama Bikira Maria mtukufu alivyoinuliwa kufikia hadhi ya kuwa Mama wa Mfalme wa wafalme, hakuna sababu yoyote ya msingi kwa kanisa kushindwa kumpa Mama huyu heshima stahiki, na kuwaalika wote wamheshimu kama Malkia, siyo tu wa mbinguni bali pia hapa duniani.

"Kama **Mwanae ni Mfalme" anatuambia Mt. Athanasio "Mama aliyemzaa ni vema na haki, tena kweli afikiriwe kuwa Malkia mwenye mamlaka."** "Mara tu Maria alipokubali kuwa Mama wa Neno wa Milele," anatuambia Mt. Benard wa Sienna**, "kwa ukubali wake, alistahilishwa kuvikwa hadhi ya umalkia wa dunia na wa viumbe vyote."**

**Mt. Athanas anahitimisha akisema, "Kama kulivyo na viumbe vingi, vinavyomtumikia Mungu, ndivyo kuna viumbe vingi vinavyomtumikia Bikira Maria;** kwa kuwa kama ilivyo kwa malaika na wanadamu, na vyote vilivyomo mbinguni na duniani, wako chini ya utawala wa Mwenyezi Mungu, ndivyo, hata wao wako chini ya uangalizi wa Mama Bikira Maria Mtakatifu sana.

Kwa hiyo, Mama Bikira Maria, lakini kwa faraja yetu ya kawaida, ijulikane kwamba ni Malkia mzuri,amabaye yuko tayari kutusaidia katika dhiki na shida zetu, na ndiyo maana Mama Kanisa anatualika kumsalimu Mama huyu kadri ya cheo chake: **Malkia wa Huruma.**

**"Cheo cha Malkia wa Mbinguni**: kadri ya Mt. Alberto Mkuu, "Ni tofauti sana na malkia wa dunia hii, Mama huyu ni mwingi wa Huruma na mapendo kwa maskini na wahitaji wa kila aina; kiroho na kimwili. Ukuu wa mfalme na malkia, kadiri ya Seneka, pamoja na kuwahurumia, kuwahuisha, na kuwaweka huru walio na taabu. Wakati viongozi wa kiimla katika ulimwengu huu, wanatawala kwa mabavu waliochini yao, tena kwa maslahi na faida zao, licha ya kwamba kwa asili inatarajiwa kwamba mfalme anapaswa kuwabeba watu moyoni mwake akiwahudumia.

Katika kutawadhwa kwa **mfalme, anapakwa mafuta, ishara ya Huruma,** kudhihirisha jinsi Huruma inavyohitajika kwa wale wanaotawaliwa. Wafalme wanapaswa pia kuhakikisha kuwa haki inapatikana kwa wote, ndiyo kusema kila mmoja anatendewa anavyostahili.

Ingawa Mama Maria ni Malkia kweli, **Yeye siyo Malkia wa Haki,** kwa mantiki ya kuwaadhibu wanaokosa na kuwatuza wasio na makosa.

Yeye ni Malkia wa Huruma, akinuia kuwapatia msamaha wote wanaokosa na kukimbilia msaada wake. Yeye ni msaada kwa wakosefu na wadhambi. Anawapatia amani, tena si amani ipatikanayo katika ulimwengu huu, ila amani ya Kristo inayotawala mioyoni mwa watu wanaomhitaji Mama huyu kwa msaada. Ndiyo maana Kanisa linahamasisha na kusisitiza **Mama huyu aitwe Malkia wa Huruma.**

Ni kana kwamba, Kristo Mfalme wa Haki na Huruma, amempatia nusu ya utawala Mama Maria, akijibakizia haki peke yake na Huruma akampatia Mama yake.Kristo atakuja na haki yake, Haki inayotafuta urari siku ya kifo chetu. Ni Mama Bikira Maria mpakwa mafuta ya Huruma yake kutokana na maombezi yake ya kimama kwa Mwanae Yesu Kristo.

Mt.Albert Mkuu hachelei kulinganisha historia ya Malkia Esta katika kitabu cha Esta, kama mfano wa Umalkia wa Bikira Maria Mbarikiwa sana Mama Maria! Sura ya nne katika kitabu cha Esta, tunasoma kuwa Mfalme Ahasuer alitoa waraka uliowahukumu Wayahudi wote kifo. Mordekai ambaye alimlea Esta,alimwomba Esta aingilie kati jambo hilo, ili awaokoe Wayahudi dhidi ya maangamizi yale.

Esta aliogopa kulifanyia kazi ombi lile, akifikiri kwa kufanya vile atapoteza heshima ya umalkia,lakini Mordekai alimkumbusha kuwa **Mungu alimpatia heshima hiyo ya umalkia kama chombo kiteule cha kuwaokoa watu.** “Usifikiri kuwa, wewe peke yako kati ya Wayahudi utaokoka kwasababu unaishi katika Kasri ya Mfalme. “Ndipo Esta akasimama mbele ya Mfalme Ahasuers akawaombea watu wake: “Ikiwa inapendeza machoni mwako, Ee Mfalme, nakuomba uwaachilie watu wangu. “Mfalme kwa kumpenda Esta, alisikiliza ombi lake na akatengua hati ya maangamizi na kutoa hati nyingine ya kuwaweka huru wana wa Israeli.

Inawezekanaje Mungu, akatae sala za Maria,ambaye anampenda upeo kwa pendo la milele. Wadhambi na wakosefu, hata walaanifu wanaokimbilia kuomba msaada wa Mama huyu wana hakika ya kufanikiwa katika maombi hayo kwani, sala za Mama Bikira Maria zitajibiwa mara pasipo kuchelewa.

**Bikira Maria, Mama wa Mungu anafahamu kwamba anapendwa na Utatu Mtakatifu uliomchagua ampatia Nafasi ya pili ya Utatu huo mwili wa kibinadamu.** Je, inawezekana kwamba Mungu akatae sala zake? Kila sala yake, kama ilivyo katika sheria ya Bwana ni lazima ioneshe Huruma kwa ajili ya wote anaowaombea.

Mt. Benard anauliza: Kwa nini Kanisa limwite Mama Bikira Maria, Malkia wa Huruma? Anajibu **"Ni kwasababu tunaamini kwamba, ni yeye anayefunua kilindi cha Huruma ya Mungu kwa yeyote anayemtaka,anapotaka,na anavyotaka ili kwamba hakuna mdhambi yeyote haijalishi ukubwa wa dhambi anayeweza kupotea ikiwa Maria atamwombea."** Huenda tukawa na mashaka wasiwasi kwamba Mama Bikira Maria haangaiki kuwaombea baadhi ya wadhambi kutokana na kufuru zao zilizojaa uasi na uhaini! Au pengine kuna wengine ambao hawapaswi kuzamishwa katika kisima hiki cha Huruma ya Mungu.

Ukweli ni kwamba, hakuna anayezuiliwa kupokea Huruma ya Mungu kupitia sala za Mama Bikira Maria. Baba Mt.Gregory wa VII anasema: "Kwa wale walio watakatifu na wachaji zaidi, huongeza ari ya Bikira Maria katika wema na Huruma kwa ajili ya wadhambi, ikiwa watamkimbilia kwa usaidizi."Tuaweza kuendelea kusema pamoja na Mt.Benard kuwa: Kwanini binadamu dhaifu na wadhambi waogope kumkimbilia Mama Bikira Maria? Kwake hakuna ugumu, wala tishio, ila uzuri,wema na hujitoa kuwasaidia wote."

Suetonius anamhusianisha Mfalme Mkuu Tito, kwamba hakuweza kumkatalia mtu yeyote chochote, kinyume chake alihaidi kuliko alivyoweza kutoa. Alitamani kwamba mwanamfalme asimuage yeyote aliyefika pasipo kuridhika kwa huduma zake.

Malkia wetu hadanganyi, na anaweza kuwapatia chochote wale wote wahitajio na kuomba. Mdhambi anayefanya toba anapomkaribia, mfanyatoba huyu anaweza kuwa na uhakika kwamba maombi yake yatasikilizwa**. "Ni nani aliyemdau wa kupokea Huruma ya Mungu ikiwa si wadhambi na wakosefu,"** anauliza Mt.Bonaventure. Utuhurumie sisi wakosefu, Ee Malkia wa Huruma, na utusaidie bondeni huku kwenye machozi kuelekea katika uzima wa milele.

**"Usinikatalie, Ee Bikira Mtakatifu,"** anasema Mt. Gregory wa Nicomedi, "Kwamba huwezi kunisaidia kutokana na dhambi zetu, kwa kuwa uwezo na huruma yako haufungwi na wingi au ukubwa wa dhambi zetu. **Hakuna kinachoweza kuzuia uwezo na ukarimu wako, kwani Mungu Muumba wetu anakuheshimu kama Mama yake, na anauchukulia utukufu wako kama ni wake mwenyewe na anafurahia kutekeleza maombi yako,kana kwamba anakulipa deni alilostahili kukulipa wewe kama mama yake.**

Hili la maanisha kwamba, ingawa Bikira Maria yuko chini ya majukumu ya kudumu kwa Mwanae Yesu Kristo, kwa kuwa Mwana huyo alimchagua kuwa Mama yake, hata hivyo

hatuwezi kupinga kwamba, Mwanae Yesu Kristo, anawajibika kwake kwani kupitia Mama huyu, alijipatia mwili na ubinadamu wake, na kwa sababu hiyo, kama fidia na kwa heshima, Yesu anamsikiliza Mama yake kwa chochote aombacho**, na kwa kumtukuza Mama yake anajitukuza mwenyewe,** ndiyo maana, anamheshimu Mama yake, kwa ajili ya wanadamu ambao sasa Yeye(Maria) ni mama yao.

Tunawezaje, katika hili kuwa na hakika kwamba Malkia huyu anaupendeleo wa hali ya juu kutoka kwa Mungu kwa ajili yetu sisi wanadamu? Tusitilie shaka au wasiwasi kuhusiana na ukweli huu. Yeye ni MAMA. Mama Mtakatifu sana, Bikira Maria ni mwingi wa Huruma na anapenda sisi tushiriki katika Huruma yake. Hakuna yeyote anayeishi katika dunia hii amabaye hakustahilishwa kupokea Huruma na upendeleo wa Mama huyu.

Mama, Bikira Mbarikiwa sana, Maria, alimfunulia Mt.Brigita anaposema: **"Mimi ni Malkia wa mbinguni na Mama wa Huruma."** Mimi ni furaha ya wenye haki, na mlango ambao wadhambi wanaingia kwenda kwa Mungu. Hakuna mdhambi duniani, haijalishi aina ya dhambi au uhaini aliotenda utakaomfanya asistahili kupokea Huruma ya Kristo kupitia sala zangu.

## SALA

Ee Mama wa Mungu na Mama yangu, kama mwombaji ninajileta mbele yako, wewe uliye Malkia wa mbingu na dunia. Kutokana katika ukulu wa kiti chako cha huruma, usisite kunitazama mimi mdhambi, Mwenyezi Mungu amekushehenisha utajiri ili uwatajirishe maskini, na amekufanya wewe kuwa Mama wa Huruma ili uwasaidie wanyonge, maskini ni wadhambi wanaotaabika katika ulimwengu huu. Natambua kuwa sistahili chochote kwa haki,na kwamba ninastahili kukosa msaada kutokana na kukosa shukrani kwa neema nyingi za Mungu nilizochezea. Kwa huruma yako, unichukue mimi na kunifanya mmoja wa watumishi wako wnaochuchumia msaada wako wa Neema za Mungu. Mama mtukufu, Malkia wa ulimwengu, unisaidie mimi katika shauku ya kukutumikia Wewe kwa uaminifu. Amina.